بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ مِنكُمْ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِى ٱلْأَرْضِ كَمَا ٱسْتَخْلَفَ ٱلَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ ٱلَّذِى ٱرْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّنۢ بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِى لَا يُشْرِكُونَ بِى شَيْـًٔا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْفَٰسِقُونَ﴾

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Wilayah Sudan**

**Jumatano, 26 Shawwal 1441 H** | **17/06/2020 M** | **Na: HTS 1441 / 55**


Tanzia kwa Mbebaji Ulinganizi

[ولَنَبْلُوَنَّكُم بِشَيْءٍ مِنَ الْخَوْفِ وَالْجُوعِ وَنَقْصٍ مِنَ الْأَمْوَالِ وَالْأَنْفُسِ وَالثَّمَرَاتِ وَبَشِّرِ الصَّابِرِينَ]

**"Hapana shaka tutakujaribuni kwa chembe ya khofu, na njaa, na upungufu wa mali na watu na matunda. Na wabashirie wanao subiri"**
(Imetafsiriwa)

Kwa macho na nyoyo zilizojawa na machozi zilizo ridhia qadhaa ya Mwenyezi Mungu, Hizb ut Tahrir / Wilayah ya Sudan inaomboleza msamaha kwa Sheikh (kwa idhini ya Mwenyezi Mungu):

**Mohammed Al-Sayir Omar**

Ambaye alitumia ujana wake katika kulingania kuregesha maisha kamili ya Kiislamu kupitia kusimamisha Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya Utume na kufanya kazi maisha yake yote ili kunyanyua bendera ya *la ilaha illa Allah Mohammed Rasulullah* (saw) (Hakuna Mola Apasaye Kuabudiwa kwa Haki Isipokuwa Mwenyezi Mungu na Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw)) kwa subira, akipitia madhara aliyo yapata akiwa katika magereza ya madhalimu na vituo vyao vya uzuizi ili kuunga mkono haki bila ya kuchoka wala kuchoshwa hadi akatimiza muda maalum hapa ulimwenguni jana asubuhi, Jumanne, 25 Shawwal 1441 H sawia na 16/6/2020.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu amrehemu na kumsamehe na kumweka katika mabustani yake mapana ya Pepo pamoja na mitume, waumini na mashahidi na watu wema kwani hakika hao ndio marafiki wazuri, na kutupa sisi na familia yake subira na faraja njema. Wanaume hufa lakini matendo yao mema hubakia na kuzungumzia utukufu wa vyeo vyao katika hali tofauti tofauti.

[إنَّا للهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ]

**"Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake Yeye hakika tutarejea"**

**Ibrahim Othman (Abu Khalil)**
**Msemaji Rasmi wa Hizb it Tahrir**
**katika Wilayah Sudan**


**Simu:** 0912240143- 0912377707

**Pepe:** Spokman_sd@dbzmail.com

**Tovuti:** www.hizb-sudan.org

**Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:** www.hizb-ut-tahrir.org

**Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:** www.hizb-ut-tahrir.info